



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA SAME.



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same anatangaza nafasi tano(5) za kazi. Maombi ya kujaza nafasi yoyote kati ya hizo yanakaribishwa kutoka kwa Mtanzania yejote mwenye sifa zilizotajwa katika tangazo hili.

1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III – (NAFASI 1)

SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI).
 - Awe amehitimoo mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa Kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU:

- i) Atakuwa ni Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa serikali ya Kijiji.
 - ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora Katika Kijiji.
 - iii) Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
 - iv) Kuwa katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
 - v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu katika Kijiji.
 - vi) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza

[Signature]

mikakati ya kuondoa umaskini, njaa na kuongeza uzalishaji mali.

vii) Kusimamia , kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji

viii) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.

Ngazi ya Mshahara: TGS B

2. DEREVA DARAJA LA II - (NAFASI 4)


A) SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (form IV) na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali.
- Waombaji wenyе cheti cha Majaribio ya Ufundı Daraja la II watafikitriwa kwanza.

B) MAJUKUMU YA KAZI.

- i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari,
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi,
- iii) Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari,
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi) Kufanya usafi wa gari,
- vii) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

Ngazi ya Mshahara: TGS B



Signature of the author, written in blue ink.

Ms. No. 00000000000000000000000000000000
NAME

UTARATIBU WA UOMBAJI:

- Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Same.
- Barua za maombi ziambatishwe na nakala za Vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi (Passport size).
- Barua za maombi ziambatishwe na maelezo Binafsi ya Mwombaji (CV).
- Waombaji waliosoma Nje ya Nchi waambatishe uthibitisho wa Vyeti vyao kutoka Baraza la Mtihani la Taifa (NECTA).
- Waombaji wote wanatakiwa wawe na umri kuanzia miaka 18 na umri usiozidi miaka 45.
- Waombaji wote waliokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili
- Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (original Certificate)
- Waombaji waandike anuani zao kwa usahihi na namba zao za simu

N.B: Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME
S.L.P 138,
SAME.**

- ❖ Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **10.09.2021** saa 9:30 Alasiri.


**Anastazia Tutuba
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SAME.**


**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
SAME**